HOTUBA YA MHESHIMIWA KASSIM M. MAJALIWA (MB,), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI AKIZINDUA SOKO LA MADINI YA DHAHABU LA MKOA WA GEITA TAREHE 17 MACHI 2019

SALAMU

Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko (Mb.), Waziri wa Madini;

Mheshimiwa Mhandisi Robert Luhumbi, Mkuu wa Mkoa wa Geita;

Prof. Simon Msanjila, Katibu Mkuu Wizara ya Madini;

Ndugu Denis Bandisa, Katibu Tawala Mkoa wa Geita;

Prof. Idris Kikula, Mwenyekiti wa Tume ya Madini;

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya;

Makatibu Tawala wa Wilaya;

Wakurugenzi wa Wilaya;

Watendaji wa Wizara na Tume ya Madini;

Wawakilishi wa wachimbaji Madini;

Wanahabari;

Wageni Waalikwa;

Mabibi na Mabwana;

Habari za Asubuhi

SHUKRANI NA PONGEZI

Ndugu wananchi,

Nianze kwa kuushukuru Uongozi wa Mkoa wa Geita, Wizara ya Madini na Tume ya Madini kwa kunialika kuwa mgeni rasmi katika shughuli hii ya uzinduzi wa Soko la Madini ya Dhahabu la Mkoa wa Geita.

Pokeeni salamu kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Viongozi wetu hao wanawasalimu na kuwapongeza kwa kazi nzuri hususan katika kutekeleza kwa wakati maelekezo, mipango na miongozo mbalimbali inayotolewa na Serikali.

Niupongeze uongozi wa Mkoa kwa kutekeleza kwa haraka kuanzisha soko mara baada ya agizo lililotolewa na Mheshimiwa Rais siku ya tarehe 22.01.2019.

MCHANGO WA SERIKALI KATIKA UKUAJI WA SEKTA YA MADINI

Ndugu Wananchi,

Tangu iingie madarakani, Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kujipambanua kuhusu dhamira yake ya kuhakikisha sekta ya madini inakua, inanufaisha watanzania pamoja na kuchangia ukuaji wa pato la taifa. Aidha, Serikali imeendelea kutekeleza maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015 – 2020 ambayo yanaitaka Serikali kubuni na kutekeleza mikakati mahsusi itakayowezesha kupunguza au kukomesha kabisa vitendo vya utoroshaji madini kwenda nje ya nchi na biashara haramu ya madini nchini.

Kwa kuzingatia hilo, Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kutoa kipaumbele katika kulinda rasilimali za madini na kuhakikisha zinawanufaisha watanzania kupitia kutungwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusiana na Umiliki wa Maliasili Namba 5 ya Mwaka 2017; Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi Katika Mikataba ya Maliasili za Nchi Namba 6 ya Mwaka 2017 pamoja na kufanya marekebisho ya Sheria ya Madini Sura 123.

Aidha, Serikali imefuta baadhi ya tozo ambazo zilikuwa kero kwa wafanyabiashara ya madini hususan wachimbaji wadogo. Miongoni mwa tozo ambazo tayari zimefutwa ni Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na Kodi ya Zuio ya asilimia tano ya mwisho (final withholding tax) inayotozwa kwenye bei ya kuuzia madini ya aina zote.

Ndugu Wananchi,

Serikali inataraji kuwa kufutwa kwa kodi na tozo hizo kutapunguza utoroshwaji wa madini; kutasaidia wachimbaji wadogo kutambuliwa kupitia uanzishwaji wa masoko ya madini; kupunguza gharama za uendeshaji wa shughuli za wachimbaji wadogo na kuongeza wigo wa mapato kwa nchi. Nitoe wito kwa wachimbaji wote wadogo kwamba endeleeni kushirikiana na Mamlaka mbalimbali za Serikali katika kutekeleza majukumu yenu kwa kufuata taratibu, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali inayotolewa na Serikali.

Ndugu Wananchi,

Serikali inachukua hatua zote hizo si kwa lengo jingine bali kuziba mianya ambayo imekuwa chanzo cha utoroshwaji wa madini, ukwepaji kodi, na hivyo, kusababisha biashara nzima ya madini kufanyika kiholela katika maeneo mengi ya nchi yetu. Napenda kuwahakikishia kwamba Serikali imejipanga vema katika kuhakikisha vikwazo vyote vilivyomo katika mnyororo wa biashara ya madini vinaondolewa kwa lengo la kukuza sekta hii na kuwanufaisha watanzania mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

UMUHIMU WA MASOKO YA MADINI NCHINI

Ndugu Wananchi,

Kama nilivyotangulia kueleza, Serikali imeamua kutoa mwelekeo mpya katika usimamizi na maendeleo ya sekta ya madini. Utekelezaji wa dhamira hii unakwenda sambamba na kuweka mazingira mazuri na miundombinu itakayowezesha kuimarika kwa sekta ya madini nchini. Moja ya miundombinu hiyo wezeshi, ni Soko hili tunalolizindua hii leo.

Ndugu Wananchi,

Mheshimiwa Alhaj Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliwahi kusema kwamba **“biashara ni kuuziana na kununuliana”**. Kwa msingi huo, Soko hili la kihistoria, litakuwa kiungo muhimu cha kuwakutanisha wachimbaji na wafanyabiashara kwa lengo la kuuza na kununua madini.

Natambua kwamba Wizara na Tume ya Madini zimeandaa utaratibu maalumu kupitia Kanuni za uanzishwaji masoko haya lakini, naomba niseme machache tu kuhusu faida zitakazopatikana kwa kuanzishwa masoko ya namna hii:-

Mosi, wachimbaji wadogo wamekuwa wakilalamikia ukosefu wa masoko ya uhakika ya madini ambao umekuwa sababu ya utoroshwaji madini. Hivyo, kuanzishwa kwa soko hili kunawahakikishia wachimbaji wadogo masoko na kipato kutokana na shughuli za madini.

Pili, kwa muda mrefu sasa, kumekuwepo na malalamiko ya kudhulumiwa au kupunjwa kutoka kwa baadhi ya wachimbaji wadogo. Vitendo hivyo vya dhuluma vimekuwa vikiwahusisha wafanyabiashara wa madini wasiokuwa waaminifu. Ndugu wachimbaji wadogo, soko hili linakwenda kuwa mwarobaini wa tatizo hilo kwani litasheheni vifaa vya kupimia uzito na ubora wa madini kabla hayajauzwa. Naielekeza Tume ya Madini, kuhakikisha inasimamia ipasavyo vifaa na taratibu nzima za vipimo kwenye soko hili na kuhakikisha kwamba hakuna manung'uniko juu ya utendaji kazi wa vifaa hivyo.

Tatu, soko hili pia litaondoa uwezekano wa wanunuzi wa madini kuibiwa na wajanja wachache wanaojifanya kuwa na madini wakati hawana. Nawasihi wanunuzi wa madini kulitumia soko hili kikamilifu ili kuepuka udanganyifu na matapeli.

Nne, vilevile, Tume ya Madini itaratibu bei za madini ndani ya soko hili na kuhakikisha mchimbaji anapata stahiki zake, Serikali inapata mapato yake na mfanyabiashara naye ananufaika. Tunaimani kabisa tatizo la kudhulumiana na kupunjana linaenda kwisha kabisa. Na kwa kweli ikitokea mtu amepunjwa, atakuwa amejitakia mwenyewe.

Tano, ndani ya soko hili kutakuwa na huduma zote muhimu kwa mfanyabiashara ikiwemo huduma za Tume ya Madini, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mabenki na nyinginezo. Kwa kifupi soko hili litatoa huduma za **one stop center** na hivyo, kuokoa muda na gharama nyingine katika kuendesha biashara hii ya madini.

Mwisho, Soko hili litasaidia sana katika kukusanya mapato ya Serikali na takwimu za biashara ya madini. Hivyo, niwasihi wachimbaji wa madini kulitumia soko hili na kuacha vitendo vya utoroshaji wa madini. Serikali kwa upande wake, haitomvumilia mtu yeyote yule atakaye jihusisha na utoroshaji wa madini.

Ndugu Wananchi,

Ni matumaini yangu kuwa masoko ya aina hii yatakuwa na tija kubwa hivyo tuna wajibu wa kuhakikisha kuwa Soko hili na masoko mengine yatakayoanzishwa yanastawi na kuwanufaisha walengwa.

MAELEKEZO YA MHESHIMIWA WAZIRI MKUU

Ndugu Wananchi,

Nyote mtakubaliana nami kuwa soko hili lina faida lukuki tena zenye kuzingatia maslahi mapana ya Taifa letu. Binafsi ninaamini kuwa endapo tutafanikiwa kufikia malengo ya kuanzishwa kwa soko hili, tutakuwa tumefanya mapinduzi makubwa kwenye sekta ya madini ndani ya muda mfupi. Hivyo, katika kuhakikisha soko hili linafikia malengo ya kuanzishwa kwake, ninaelekeza kama ifuatavyo:-

Moja, Wizara na Tume ya Madini, shirikianeni na Serikali ya Mkoa, kusimamia soko hili kikamilifu na kwa ufanisi ili lilete manufaa yanayokusudiwa.

Pili, Wizara na Tume ya Madini kamilisheni ufungaji wa vifaa vyote muhimu, miundombinu na uwepo wa rasilimali watu ya kutosha ili soko hili lifanye kazi kwa ufanisi na kama ilivyokusudiwa.

Tatu, Wizara iendelee kushirikiana na wadau wote muhimu kuandaa utaratibu maalumu wa kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo kuhusu namna soko linavyofanya kazi, faida zake na mambo mengine yatakayolitangaza soko hili kwa mchimbaji na mfanyabiashara na hivyo kulitumia soko ipasavyo;

Nne, viongozi na watendaji wote wa Serikali simamieni kwa weledi, uaminifu na uadilifu, sheria, kanuni na miongozo ya Serikali kuhusu sekta hii ya madini kwa lengo la kudhibiti utoroshwaji wa madini hususan dhahabu kwenda nje ya nchi. Nitoe tahadhari kwa wadau wote wa madini kuwa atakayekamatwa anatorosha madini, atachukuliwa hatua za kisheria ikiwemo utaifishaji wa madini atakayokuwa akiyatorosha.

Tano, Wizara ya Madini, Tume ya Madini, Serikali ya Mkoa, Idara na Taasisi nyingine za Serikali zinazohusika na maendeleo ya sekta hii ya madini hakikisheni mnaheshimu mipaka ya majukumu yenu ili muweze kulisimamia vizuri soko hili na kufanya kazi kama ilivyokusudiwa.

Sita, Wizara ya Madini ishirikiane na Vyama na Mashirikisho ya wachimbaji na wafanyabiashara wa madini kuandaa Mpango Kazi mahsusi kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya soko hili ili lisigeuke kuwa kikwazo kipya kwa wachimbaji na wafanyabishara wa madini. Wizara, Mikoa na KUU zisimamievyama vya wachimbaji hasa vya wachimbaji wadogo. Mara kadhaa wachimbaji wa kati wamekuwa wanalalamika kupata uongozi kwa wachimbaji wadogo. Hata pale wachimbaji wadogo wameunda uongozi, wachimbaji wa kati huanzisha mgogoro ili washike wao. Iko migogogro inapangwa kufanyika: Nyakafuru, Ikuzi, Bingwa, Gasuma. Wachimbaji wadogo waachw waunde uongozi wao.

Saba, Idara na Taasisi zote za Serikali zinazohusika na uwekaji wa miundombinu wezeshi kwenye soko hili, shirikianeni na Wizara ili soko hili liweze kustawi.

Nane, Vyombo vya Ulinzi na Usalama hakikisheni soko hili linapata ulinzi wa kutosha muda wote, ili watendaji, mali zitakazokuwemo, vitendea kazi na miundombinu yote iwe salama muda wote. Mkuu wa mkoa na Wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama, nawaagiza hakikisheni Suala hili mnaliandalia utaratibu haraka iwezekanavyo.

Mwisho, nitumie fursa hii kuielekeza mikoa mingine yenye kiwango kikubwa cha uzalishaji wa madini hususan ya metali na vito iharakishe uanzishwaji wa Masoko ya madini sanjari na miundombinu yote muhimu ili masoko hayo yaanze kufanya kazi kabla ya kwisha kwa mwaka huu wa fedha 2018/2019.

Ndugu Wananchi

Ninayo imani kubwa kwamba, usimamizi mzuri wa soko hili na masoko mengine ya madini yanayoendelea kuanzishwa nchini utaimarisha makusanyo ya kodi za Serikali na kuongeza mchango wa sekta hii kwenye pato la Taifa. Vilevile, wafanyabiashara wa madini, hususan kutoka nje ya nchi, wataongezeka kwa sababu tutakuwa tumewaepusha na matapeli na vikwazo vingine vya kibiashara. Uimara wa soko hili pia, utaboresha uhusiano kati ya wadau wa biashara ya madini na Serikali.

HITIMISHO

Ndugu Wananchi,

Kama mtakavyoona, lengo la Serikali kuanzisha masoko ya madini ni zuri na lina maslahi mapana ya nchi. Hivyo ni vyema tukahakikisha kwamba kwa pamoja, tunayalinda masoko haya, tunayatetea na tunayawezesha kwa kadri tunavyoweza. Kwa upande wa Serikali, itahakikisha masoko haya yanaendeshwa kwa njia shirikishi, uwazi na uadilifu ili sote kwa pamoja tunufaike nayo.

Mwisho, nimalizie kwa kuwashukuru wote kwa kufika kwenye shughuli hii muhimu, na kwa kuunga mkono jitihada hizi ambazo Mheshimiwa Rais wetu amezipigania na hatimae leo tunashuhudia kuzinduliwa kwa Soko la madini katika Mji wa Geita. Hongereni sana wanaGeita.

Ndugu Wananchi,

Baada ya kusema hayo, sasa nipo tayari kuzindua rasmi Soko la Madini Geita.

AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA